**12C-Swifaatul-llatiy Laa Dhwidda Lahaa (Swiffah Zisizokuwa Na Kinyume Chake)**

**B- صِفاَتُ الَّتِي لاَ ضِد لهَا Swifaatul-llatiy laa dhwidda lahaa - Swiffah Zisizokuwa Na Kinyume Chake**

1. **الصَّفِير Asw-Swafiyr – Mluzi:**

Sauti yenye kushabihiana na sauti ya ndege, itokayo baina ya ncha ya ulimi na meno na hivyo sehemu itokayo ni ya kudhikika. Au mfano wa sauti ya mluzi inayofanana na birika lenye mdomo mdogo yanapochemka maji. Au mfano sauti ya mvumo wa mbu au nzige; sauti yenye kufuatana na kutamka kwa herufi moja katika herufi tatu hizi: ص س ز ; na mluzi huwa zaidi wakati wa sukuwn. Sauti ya ز ikiwa ni yenye kuvuma zaidi kama mbu.

2. **الْقَلْقَلَة Al-Qalqalah – Kugonga Kwa Kutetema:**

Kugonga kwa kutetema au kuachilia makhraj ya herufi wakati wa kuitamka hali ya kuwa na sukuwn mpaka ikasikika *nabrah* (kugongeka) yake yenye nguvu; herufi zake ni tano (5) zilizojikusanya katika ibara: swiffahkatika herufi hizi kwa kuwa zina gongaHuwajibika ku. **قُطْبُ جَدّ**[1] mbili, nazo ni **الْجَهر** Al-Jahr na **الشِّـــدَّة** kwa vile swiffah ya **الْجَهر** inazuia pumzi wakati wa kutamka herufi, na swiffah ya **الشِّـــدّة** inazuia sauti wakati wa kutamka herufi, hivyo ndio ikawa hapana budi isipokuwa kugongeka makhraj ili ipate kudhihiri sauti ya herufi.

3. **اللِّين Al-Liyn** - **Laini:**

[1] Rejea mlango wa 'Qalqalah'

Kutamka herufi kwa ulaini bila ya kukalifisha ulimi yaani bila ya mashaka. Herufi zake ni و na ي zikiwa na sukuwn na zilizotanguliwa na *i'raab* ya fat-hah[2]

4. **الإنْحِرَاف Al-Inhiraaf - Kugeuza:**

Kuelemea herufi baada ya kuitamka katika makhraj yake na kufikia makhraj nyingine. Inatokea katika herufi mbili ر na ل. Herufi ya ر inatamkwa ikielekea katika makhraj ya ل na hali kama hiyo hutokea inapotamkwa herufi ya ل kwamba inaelemea katika makhraj ya ر.

5. **التَّكْرِير At-Takriyr - Kukariri:**

Nayo ni wwiffah ya herufi moja tu, herufi ya ر ; na kusudio lake ni kujiepusha nayo kwani herufi ya ر inakubali kukariri kwa kupinda ncha ya ulimi wakati wa kuitamka, hivyo basi kila inapopinda ncha ya ulimi, mara moja hutoka herufi ya ر, na haijuzu kuitoa zaidi ya ر moja tu.

6. **التَّفَشِّي At-Tafasshiy** - **Kuenea**:

Kuenea hewa mdomoni wakati wa kuitamka herufi ya ش . Ni swiffah pekee katika herufi yake ya pekee.

7. **الإِسْتِطالِة Al-Istitwaalah - Mvuto:**

Kuvuta sauti katika makh-raj ya ض mpaka yakaunganika na makh-raj ya ل, na hujaza sakafu ya mdomo wote na sauti huendelea kutiririka wakati wa kuitamka ض kwa rakhaawatihaa (udhaifu au ulaini wake).

Herufi ya ض inatofautika na herufi nyengine zote za Kiarabu kwa kuwa na swiffah hii ya pekee ya الإستطالة al-istitwaalah (mvuto), nayo ni katika herufi ngumu, yenye mashaka na nzito sana kutamka kwa ulimi.

[2] Rejea mlango wa 'Maddul-far-'iy kuhusu maddul-liyn'

**Tanbihi:** Swiffah hizo zote zinakuwa na nguvu zaidi herufi zinapokuwa zina sukuwn, na zinapunguka zinapokuwa na *i'raab* [3]

[3] Huwa hivyo katika swiffah zote isipokuwa al-qalqalah kwa sababu ya sharti lake la sukuwn.